



Funded by the European Union



Katiba
ya Kenya 2010
imebainisha haki
ya kupata huduma
za kisheria na kutia
nguvu juhudhi mpya
za kurekebisha
mfumo wa haki

Mradi wa Uwezeshaji na Utoaji wa Misaada ya Kisheria nchini Kenya – PLEAD

Kuimarisha ufikiaji wa haki

Usuluhishi wa mizozo

Kuimarisha utoaji wa huduma za kupata haki

utumiaji wa njia mbadala ya adhabu ya kifungo



SIAYA PROBATION
FEMALE HOSTEL

Kuhusu PLEAD

Licha ya hatua zilizopigwa hivi karibuni, kupata haki bado ni changamoto nchini Kenya. Kuna vizuizi kadhaa vinavyozua upatikanaji wa usawa wa haki.

Navyo ni pamoja na:


- Mrundiko mkubwa wa kesi mahakamani hivyo kufanya mashtaka kuchukua muda mrefu
- Gharama kubwa ya mawakili na ushauri wa kisheria
- Umbali mrefu ambao wananchi wanalaazimika kusafiri ili kupata huduma za mahakama katika baadhi ya kaunti
- Athari za ufisadi na ubaguzi ambao huondoa imani ya wananchi katika mfumo wa haki
- Kutotumiwa kikamilifu kwa mfumo wa kujiweke dhamana au kudhaminiwa pamoja na mbinu nydingine badala ya kufungwa hali inayofanya magereza kujaa kupita kiasi
- Kuenea kwa mbinu mbadala za mfumo wa haki ambazo haziambatani na Haki za Binadamu katika Katiba
- Wananchi kutofahamu vizuri haki zao na utumiaji wa lugha ngumu ya kisheria inayofanya watu wengi kutopata huduma
- Uwezo mdogo wa mashirika ya kiraia (AZAKI) katika kutoa huduma za kisheria.

Wakenya wengi sana ambao hawafai kufungwa wapo gerezani, wakiwemo waliopatikana na makosa madogo lakini hawana uwezo wa kulipa faini. Isitoshe, mashirika kuu katika mfumo wa kupata haki hayaelewi majukumu yao vizuri hivyo kuathiri uwezo wa mashirika hayo kutekeleza majukumu yao.

Mradi wa Uwezesaji na Utoaji wa Misaada ya Kisheria nchini Kenya (PLEAD) ni ushirikiano unaohusisha Serikali ya Kenya, Umoja wa Ulaya, Umoja wa Mataifa na mashirika ya kiraia unaonua kuboresha utoaji wa huduma za kisheria, usuluhishi wa mizozo na utumiaji wa mbinu mbadala ya adhabu ya kifungo.

Mradi wa PLEAD ulianzishwa mwaka 2018 na umejikita katika Ruwaza ya Kenya ya 2030. Mradi huu unaunga mkono marekebisho yanayofanywa na serikali kwa lengo la kurekebisha mfumo wa haki za jinai kwa manufaa ya raia wote. Mradi huu wa Shilingi bilioni 4.2 (Yuro milioni 34.15) ndio mkubwa zaidi kufanywa na Umoja wa Ulaya katika sekta ya haki katika nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara na unaunga mkono juhudui kuu zinazofanywa na Serikali ya Kenya.

Washirika wa PLEAD




PLEAD ina asasi sita zinazoshughulikia haki za jinai - Baraza la Taifa la Utekelezaji wa Haki, Idara ya Mahakama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, Idara ya Majaribio na Huduma za Baada ya Kuhukumiwa, Idara ya Haki na Ulinzi wa Mashahidi - Umoja wa Ulaya, Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevyaa na Uhali (UNODC), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na zaidi ya Mashirika 20 ya Kiraia ambayo kwa sasa zinachaguliwa. Ushirikiano huu unatekelezwa kwa pamoja na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevyaa na Uhali (UNODC), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).



● **Kaunti zinazoangaziwa na PLEAD**

Matokeo

Washirika wa PLEAD wananuia kuwapa Wakenya matokeo manne makuu:



- ▶ **1. Kuboresha upatikanaji wa haki hasa kwa maskini na watu walio katika hatari ya kuathirika, kwa kuzingatia misaada ya kisheria** – Inajumuisha kutoa mafunzo na usaidizi wa kitaalamu kwa Idara ya Haki, Mashirika ya Kiraia katika kaunti 12 zinazoangaziwa na kutoa huduma saidizi na habari za kisheria kuititia Amkeni Wakenya.
- ▶ **2. Kuimarisha utawala wa mahakama na usimamizi wa kesi** – Mfumo bora wa usimamizi wa mashtaka utasaidia kupunguza mrundiko wa kesi na kukabiliana na ufisadi. Utungaji wa sera (ikiwemo sera na miongozo ya kwanza ya Mfumo wa Mbinu Mbadala za Haki nchini Kenya), mafunzo, miundomsingi muhimu na vifaa vya ofisi pia ni sehemu ya usaidizi wa mfumo wa Sheria.
- ▶ **3. Kuongeza ubora na ufanisi wa mfumo wa haki za jinai** – Inajumuisha usaidizi wa kuandaa mipango ya kimkakati, utungaji wa sera, mtalaa wa mafunzo, uhamasishaji na kutoa vifaa kwa ajili ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma, Idara ya Majoribio na Huduma za Baada ya Kuhukumiwa, na kwa Idara ya Haki na Ulinzi wa Mashahidi ili kuboresha utoaji wa huduma na kuwezesha kusambaa kwa mbinu zilizo mbadala za kufungwa gerezani.
- ▶ **4. Kuboresha mwingiliano na ushirikiano katika sekta nzima ya haki** – Kuweka mipango ya kimkakati na usaidizi mwiningine wa kitaalamu ili kuwezesha Baraza la Taifa la Utekelezaji wa Haki kutekeleza wajibu wake na kuunga mkono juhudii zinazofanywa ili kusuluhiha changamoto zinazokumba utoaji wa haki.

PLEAD inaunga mkono juhudii za kutimiza Lengo la 16 la Ajenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu kwa kuchangia katika kujenga taasisi za haki zilizo imara, jumuishi na zinazowajibika. Kuboresha utendaji wa haki kutaisaidia Kenya kudumisha mazingira bora ya kibiashara na hivyo kuhimiza uwekezaji na kubuni nafasi za kazi.

Kwa hakika, PLEAD inaleta tumaini kwa Wakenya wote ili wawe na imani katika mifumo rasmi na isiyo rasmi ya utekelezaji wa haki.

Kaunti zinazoangaziwa

Ingawa PLEAD inatarajia kufikia taifa zima, mradi huu umeangazia kaunti 12:

- Maeneo matano makuu zaidi ya miji – Kisumu, Mombasa, Nakuru, Nairobi na Uasin Gishu;
- Kaunti saba zilizokuwa zimetengwa – Garissa, Isiolo, Lamu, Mandera, Marsabit, Tana River na Wajir.

Haki bila kifungo gerezani

Lengo

Kupunguza
kwa asilimia
30%

idadi ya wanaozuiliwa
korokoroni kabla ya kesi
kufikia 2022 ili kupunguza
msongamano
magerezani

Upatikanaji
wa haki ni
haki ya binadamu
na ni muhimu
katika kukabiliana
na umaskini na
uwezekano wa
watu kuathirika



© Alan Gichig/U.N.D.P

PLEAD inazingatia mtazamo mpana wa mfumo wa haki unaojumuisha mbinu rasmi na za jadi zinazotumiwa kupata haki.

Uelewa mdogo wa mbinu nyingine tofauti na kufunga watu gerezani, pamoja na hali ya maofisa wa mahakama, waendesha mashtaka na polisi kutokubali kwa haraka mbinu hizo kusababisha utegemeaji mkubwa wa adhabu ya kifungo. Washirika wa PLEAD wanajitahidi kubadilisha mienendo na kuonyesha kwamba kuna njia nyingi za kupata haki.

Mbinu mbadala kama vile kuwaelekeza watu kwenye mfumo wa nje ya mahakama na kukiri kosa fulani ili kupata msamaha huwasaidia raia kupata fursa nyingine ya kuwa wema badala ya kuwa na rekodi ya uhalifu na huweka kipaumbele katika kurekebisha tabia badala ya kuadhibu, hasa kwa wanaopatikana na kosa kwa mara ya kwanza.

Kwa kuunga mkono washirika wa Mashirika ya Kiraia katika kaunti zilizokuwa zimetengwa, PLEAD inaziwezesha jamii kufikia haki kwa usawa. Juhudi hizi ni pamoja na uhamasishaji wa kuelewa mfumo wa haki na utekelezaji wa sheria, kutoa usaidizi wa kisheria kupitia wasaidizi wa kisheria waliofundishwa pamoja na mafunzo yanayoangazia haki za binadamu.

Watu walio kizuizini wakisubiri kesi au baada ya kuhukumiwa pia wanapokea usaidizi wa PLEAD kupata uwakilishi wa kisheria na kuwezeshwia.

Lengo

Kuhakikisha
kwamba angalau
asilimia
15%

ya wanaume na wanawake
waliohojiwa katika kaunti 12
zilizotengwa wanaotafuta
haki wanaweza
kuipata.



"Kwa kuunga mkono washirika wa Kiraia katika kaunti zilizokuwa zimetengwa, PLEAD inaziwezesha jamii kufikia haki kwa usawa. Juhudi hizi ni pamoja na uhamasishaji wa kuelewa mfumo wa haki na utekelezaji wa sheria, kutoa usaidizi wa kisheria kupitia wasaidizi wa kisheria walifundishwa pamoja na mafunzo yanayoangazia haki za binadamu."



Programme for Legal Empowerment and Aid Delivery in Kenya – PLEAD



Funded by the European Union



UNODC

United Nations Office on Drugs and Crime



Wasiliana na

Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kudhibiti
Dawa za Kulevyaa na Uhali (UNODC)
Tawi la Afrika Mashariki
unodc-easternafrica@un.org
www.unodc.org/easternafrica/plead/

UNDP Kenya
amkeniwakenya.ke@undp.org
www.ke.undp.org

Fuatilia washirika wa PLEAD:
#PLEADyetu
#HakilweNgao

Brosa hii ilitolewa kwa msaada wa kifedha wa Jumuiya ya Ulaya. Yote yaliyomo yametolewa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevyaa na Uhali (UNODC) na UNDP na hayaakisi maoni ya Jumuiya ya Ulaya.